**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

*[Imeandikwa kwa mujibu wa Kanuni ya 123 na kuwasilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

IDARA YA KAMATI ZA BUNGE,
S.L.P. 941,
**DODOMA**.

**Mei, 2019**

## YALIYOMO


**YALIYOMO** ............................................................................................ i

**SEHEMU YA KWANZA** ............................................................................ 1

1.0 **UTANGULIZI** ..................................................................................... 1

**SEHEMU YA PILI** .................................................................................. 3

2.0 **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020** ............................................................................ 3

2.1 Makusanyo ya Mapato ............................................................................ 3

2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2018/2019 ............................................. 3

2.3 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa kwa Mwaka 2018/2019 ............ 4

2.3.1 Yaliyobainika katika Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ..................... 5

2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ............................................ 13

2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 ............................................................................................ 18

2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ........... 18

2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ........... 18

2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 ........................................................................... 19

**SEHEMU YA TATU** ................................................................................ 32

3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ...................................................... 32

3.1 Bajeti ya Wizara ................................................................................... 32

3.2 Sekta ya Uchukuzi ................................................................................. 33

3.3 Sekta ya Ujenzi .................................................................................... 38

3.4 Sekta ya Mawasiliano ............................................................................. 42

4:0 **HITIMISHO** ....................................................................................... 46

4.1 Shukrani ............................................................................................. 46

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: -

   i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

   ii) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mambo mengine muhimu

yaliyojitokeza wakati wa kujadili, kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika **Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi)** na **Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano).**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 2.1 Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufikia 28 Februari, 2019, Sekta ya Mawasiliano ilikusanya jumla ya **Shilingi 32,094,316,287.09.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 32,093, 716, 287.09** zimetokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na **Shilingi 600,000** zimetokana na mauzo ya nyaraka za zabuni.

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 68, 827, 800.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Hadi kufika mwezi Machi, 2019 jumla ya **Shilingi 23,180,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 33.68** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa.

### 2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia 28 Machi, 2019**

| SEKTA | Fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19 | | | Fedha zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2019 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Kawaida | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo |
| Uchukuzi | 90,675,898,235 | 2,300,739,000,000 | 0 | 54,920,905,599.40 (60.56%) | 391,161,650,000 (17%) | 0 |
| Ujenzi | 33,129,943,796.00 | 1,540,514,754,141.38 | 435,927,599,000.00 | 21, 078,292,500.00 (64%) | 850,266,153,647.15 (55%) | 252,325,455,891.00 (58%) |
| Mawasiliano | 3,856,423,000 | 15,000,000,000 | 0 | 2,728,316,826.97 (71%) | 1, 531,406,368.91 (10%) | 0 |

***Chanzo: Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98), mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Sekta hii ni wakuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2019 **asilimia 55** tu ya Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo zilikuwa zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62), bado kumeendelea kuwapo kwa changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati; na hivyo, kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kuanza; hivyo, kutokukamilika kwa wakati uliopangwa. Kama Jedwali Na.1 linavyoonesha, kati ya Fedha zote za Ndani za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; fedha zilizotolewa hadi kufika mwezi Machi, 2019 ni **asilimia kumi na saba tu (17%)** tu hivyo, baadhi ya miradi haikupata fedha yoyote. Miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mtwara-M/bay, Mchuchuma & Liganga (Km 1092), ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga-Arusha hadi Musoma (Km 1,108) na mradi wa usafiri wa Treni Abiria Jijini Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), Kamati imebaini kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa hadi Mwezi Machi 2019, ni **Shilingi 3,670,500,020.00** ambapo kati ya fedha hizo, Fedha zilizotumika ni **Shilingi 1,531,406,388.91** tu.

## 2.3 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa kwa Mwaka 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi 20 Machi, 2019 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Mtwara. Miradi iliyotembelewa ni; -

a) Viwanja cha Ndege cha Dodoma na Msalato;
b) Ujenzi wa reli ya kati sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro;
c) Ujenzi wa jengo la tatu la Abiria (Terminal III), na Ujenzi wa rada ya kuongozea ndege Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
d) Chuo cha Usafirishaji Tanzania-NIT
e) Ujenzi wa barabara ya Mtwara-Newala- Masasi (km 210)
f) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara; na
g) Ujenzi wa Bandari ya Mtwara.

### 2.3.1 Yaliyobainika katika Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

i) **Mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, Dodoma**.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma zilianza rasmi mwezi June, 2018 na unatarajiwa kukamilika Machi 2019 kwa gharama ya Shilingi **milioni 624**. Mradi huu wa upanuzi na ukarabati wa jengo la abiria umeongeza ukubwa wa jengo hadi kufikia uwezo wa kuhudumia abiria 146 wanaoondoka kwa wakati mmoja ukilinganisha na uwezo wa jengo la zamani lililokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 35 tu.

Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa changamoto inayokabili upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Cha Dodoma ni upatikanaji wa fedha na gharama kubwa kwa ajili ya fidia za utwaaji wa eneo lililosalia ili kumalizia kusimika mfumo wa taa za kuongozea ndege, ambapo kwa sasa zimewekwa upande mmoja tu wa barabara ya kuruka na kutua ndege.

Aidha, Kiwanja kutokuwa na uzio huku kimezungukwa na makazi ya watu wenye shughuli mbalimbali zisizo rafiki kwa usafiri kwa anga. Jambo hili wakati mwingine linasababisha watu kukatiza Kiwanjani hapo. Juu ya hayo, mara kadhaa wanyama, kama vile, mbwa; hukatiza katika maendeo ya Kiwanja jambo linalodhoofisha usalama wa kiwanja.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu kiwanja cha ndege cha Msalato, Kamati ilijulishwa kuwa mwaka 2017, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, iliingia Mkataba na Kampuni ya STUDI *International* ya nchini Tunisia kwa ajili ya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali; na pia, kufanya usanifu wa kina katika Kiwanja hiki kwa gharama ya **Dola za Kimarekani 1, 885, 050.00.**

Kazi za usanifu zimelenga kugawa mradi katika awamu mbili; yaani awamu ya kwanza, ambapo Kiwanja kitakuwa daraja (code) 4E chenye uwezo wa kuhudumia ndege kubwa kama, Airbus A 350, Boeng 787 Dreamliner, Boeng 777, Ndege za Mizigo aina ya Antonov (AN-125) kwenye kipindi cha miaka 20 ya awali; na awamu ya pili ambayo itahusu kupanua Kiwanja kufikia

daraja (code) 4F lenye uwezo wa kuhudumia Ndege kama Boeng 747 na Airbus A380. Benki ya ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa awamu wa kwanza ambao unakadiriwa kugharimu dola za Kimarekani **Milioni 591.266.**

Katika mradi huu wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, changamoto imekuwa ni upatikanaji wa fedha za ujenzi pamoja na ulipaji fidia kwa wananchi waathirika wapatao 1,926 ambao wanatarajiwa kulipwa fidia kiasi cha **shilingi bilioni 14.6**.

ii) **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *(Standard Gauge)* sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa, Ujenzi wa Reli ya Kati sehemu ya Dar es Salaam mpaka Morogoro (Km 300) kinajengwa kwa ubia wa Kampuni ya YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA-ENGIL ya Ureno. Gharama za Mradi kwa sehemu hii ni **Shilingi Trioni 2.7**.

Shughuli zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa madaraja (42%), ujenzi wa makalvati (55%), ujenzi wa daraja refu katikati ya jiji la Dar es Salaam lenye Km 2.54 (63%), ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde (66%), kazi za utandikaji wa reli zinaendelea; pamoja na, kazi ya uwekaji wa nguzo za umeme kwa ajili ya kuendeshea treni.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, maendeleo ya mradi wa ujenzi kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni mazuri; kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mradi zinatolewa vema na kwa wakati na hakuna madai yoyote kwa Mkandarasi. Aidha, fidia mbalimbali kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli zinaaendelea kutolewa kadiri mradi unavyosogea. Ujenzi wa sehemu hii umefikia asilimia 45, na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Novemba, 2019.

iii) **Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria *(Terminal III),* Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa mkandarasi wa ujenzi na mhandisi mshauri walipatikana mwaka 2013 na wameendelea na kazi za ujenzi kwa kuzingatia mikataba yao na Serikali. Hadi mwezi Februari 2019, utekelezaji wa kazi zote umefikia asilimia 95. Kasi hii imetokana na juhudi za Serikali kulipa madai ya mkandarasi kwa lengo la kumaliza kazi kwa muda uliopangwa.

Kwa ujumla, mchanganuo wa kazi zote za ujenzi wa jengo zimefikia asilimia tisini na sita (96%), kazi za nje ya jengo – (maegesho ya magari) asilimia tisini na mbili *92%,* kazi za nje ya jengo *(*maegesho ya ndege) asilimia tisini na nane (98%). Kazi za ujenzi zinaendelea vizuri na inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Mei, 2019.

Kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja hiki kutawezesha kuhudumia abiria 2,800 kwa saa; na abiria milioni sita, kwa mwaka, jambo litakalosababisha kiwanja hiki kuwa kitovu cha usafiri wa anga nchini na Afrika mashariki kwa ujumla.

iv) **Ujenzi wa Rada ya Kuongozea Ndege**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha usafiri wa anga nchini, mwaka 2016/17, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ilianza mchakato wa ununuzi wa rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia nchini. Mradi huu unatekelezwa na Mzabuni Thales LAS France SAS kutoka Ufaransa kwa thamani ya ***Euro 22, 351,248.00*** gharama ya mitambo na **Shilingi 5, 865,097,261** gharama ya ujenzi wa miundombinu.

Mradi wa Rada unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100; ambapo asilimia 55 sawa na **Shilingi bilioni 35.1** imegharamiwa na Serikalili Kuu. Fedha hizi zimekwishapokelewa na Mamlaka. Aidha, Mamlaka inagharamia asilimia 45 sawa na **Shilingi bilioni 27.3.**

Usimikaji wa rada hizi unahusisha viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, Kilimanjaro na Songwe-Mbeya. Mpaka mwezi Machi 2019, jumla ya **Shilingi**

**Bilioni 57,322,085,709** zimekwishatumika kwa manunuzi ya Rada nne na ujenzi wa jengo la Rada. Hatua za utekelezaji zilizofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 100 jengo la mnara wa Rada, kibanda cha Mlinzi, na jengo la mitambo ya rada. Aidha, Usimikaji wa mtambo unaoendelea umefikia asilimia 90%.

v) **Chuo ha Taifa cha Usafirishaji-NIT**

**Mheshimiwa Spika,** kwa uwekezaji huu mkubwa unafanywa na Serikali katika Sekta Usafiri na usafirishaji. Hata hivyo, ipo haja ya kuhakikisha uwekezaji mkubwa pia unafanyika katika uandaaji wa rasilimali watu watakaoendesha na kusimamia uwekezaji huo. Kamati ilipotembelea Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ilibaini changamoto mbalimbali ambazo kimsingi zikifanyiwa kazi zitasaidia Chuo hiki kufanya kazi vizuri zaidi na kuzalisha wataalam wengi watakaosaidia kusimamia na kuendeleza miundombinu nchini. Changamoto hizo ni; -

a) Upungufu wa Watumishi 133 (wanataaluma 87 na watumishi wa kawaida 46). Hali hii imesababisha chuo kutumia watumishi wa muda kutoka nje hasa wanataaluma jambo lenye gharama kubwa na kuelemea Chuo;
b) Madeni ya Chuo ya Mwaka 2015/16 yanayofikia **Shilingi Bilioni 2.29** yanasuburi kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani Serikali;
c) Upungufu wa Vifaa vya kujifunzia na kufundishia hasa mafunzo ya uhandisi;
d) Kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi wa jengo la Rasilimali Mafunzo (Maktaba), chuo kimeshindwa kukamilisha ujenzi wa awamu ya tatu wa kituo kama ilivyopangwa kutokana na ufinyu wa bajeti; na
e) Uhaba wa hosteli za wanafunzi, uchakavu wa barabara za ndani ya chuo, uhaba wa miundombinu ya chuo kama vile, madarasa, karakana na ofisi za watumishi;

vi) **Barabara ya Mtwara-Newala Masasi**

**Mheshimiwa Spika**, barabara hii ni kati ya barabara za kiuchumi Mkoani Mtwara ambayo inaanzia Mtwara Mjini – Newala – Masasi Km 210) kwa kupitia Wilaya za Tandahimba na Newala. Ni dhahiri kuwa Serikali iliona umuhimu wa kuijenga barabara hii kimkakati kutokana na uzalishaji mkubwa wa zao la korosho ambao hufanyika katika maeneo inayopita barabara hii.

Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 19 Januari, 2017 na kazi ilianza kutekelezwa rasmi tarehe 17 Aprili, 2017. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani kati ya Kilometa 210, za barabara hii zimejengwa Kilometa 50 tu tangu Mwaka 2017 ambazo ujenzi wake umefikia asilimia 38 tu.

vii) **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara ulisainiwa tarehe 09 Novemba, 2017 kati ya Serikali ya Tanzania na *M/S Beijingh Consruction Engineering Group Company* Ltd kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 50.4** kwa muda wa miezi 27. Kwa mujibu wa Mkataba, kazi zinatarajiwa kukamilika 26 Septemba 2020. Hali ya kiwanja hiki kwa sasa ni chakavu kutokana na kuwepo kwa mashimo na kubonyea kwa tabaka la lami. Serikali imekusudia kupanua kiwanja hiki kutoka daraja la 3C kwenda 4E ili kiweze kuhudumia ndege kubwa zaidi ndani na nje ya nchi kutokana na umuhimu wa hasa wa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2018/2019, kiwanja hiki kilitengewa jumla ya **Shilingi 12,848,000,000.00.** Mkandarasi amewasilisha ombi la kulipwa malipo ya awali **Shilingi 7,008,497,029.91** ambapo Kamati imejulishwa kuwa Wizara ya Fedha inaendelea kukamilisha taratibu za malipo hayo. Hata hivyo, mradi huu umechelewa kuanza kwani Mkataba wa ujenzi ulisainiwa toka mwaka 2017 ambapo unatakiwa 2020. Kamati inaona ipo haja ya Mkandarasi kuongeza kasi ya ujenzi ili kukamilisha mradi kwa wakati.

viii) **Bandari ya Mtwara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, bandari ya Mtwara ilijengwa katika miaka ya 1950 ikiwa na uwezo wa kuhudumia tani 400,000 za shehena kwa mwaka. Hata hivyo, bandari hii imeendelea kuwa ya umuhimu katika ukanda wa kusini kwa kupitisha shehena za korosho zisizobanguliwa, makasha, saruji, mitambo na bidhaa zinazotumika katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi baharini.

**Mheshimiwa Spika**, Kijiografia bandari ya Mtwara inazo fursa nyingi kutokana na kuwa na kina kirefu cha mita 9.5 hadi mita 12.5 katika baadhi ya maeneo, eneo kubwa la upanuzi ikilinganishwa na Bandari jirani za Nacal, Beira na Durban zinazotumiwa haswa na nchi za Malawi na Msumbiji. Fursa hizi zinaweza kuongezeka endapo; -

a) Bandari itaunganishwa na reli/barabara kutoka Mtwara hadi Mbambabay kwa mizigo ya nchi za Malawi na Zambia; na

b) Miundombinu ya Bandari itaboreshwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Gati mpya za nyongeza;

**Mheshimiwa Spika,** endepo Bandari hii itaimarishwa itasaidia sana kupata mzigo nchi ya Malawi, kwani karibu migodi yote mikubwa ya madini iko Kaskazini mwa nchi hiyo, hivyo bandari ya Mtwara ndiyo itakayokuwa njia fupi zaidi kuliko bandari za Afrika ya Kusini, hususan Durban.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mipango ya kupanua bandari ya Mtwara kwa kujenga gati nne mpya na kuifanya kuwa ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shehena ya gesi na mafuta, madini, na mazao ya kilimo yanayopatikana ukanda wa Mtwara. Ujenzi kamili ulianza mnamo tarehe 27 Mei 2017 ambapo kwa sasa umefikia asilimia 35 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotembelea mradi huu, ilijionea maendeleo na kasi nzuri ya utekelezaji. Yapo mapungufu yaliyofanyika mwanzoni mwa mradi ambapo mradi ulianza bila ya kuwa na Mshauri Mwelekezi; hivyo kusababisha kujenga/ kuchimba kina cha Mita 13 badala ya 15 na upana wa mita 5 badala ya mita 5.5.

ix) **Mradi wa Anuani za Makazi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mtaa wa Uhuru na kuona utekelezaji wa mradi huu unavyoendelea. Kamati ilielezwa kuwa ifikapo mwezi Aprili, 2019 miundombinu itakamilika katika Kata 3 ambapo inatarajiwa Kata husika zianze kutumia anwani za makazi kufikisha huduma mahali alipo mwananchi ama taasisi kupitia huduma za Posta Mlangoni na EMS.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo huu unalenga kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na anwani ya makazi; hivyo, kuwezesha mwananchi kuhudumiwa kirahisi mahali alipo. Manufaa mengine ya mfumo huu ni kama yafuatayo: -

i) Kuongeza ajira kutokana na fursa za kusambaza bidhaa kwa wateja;

ii) Kurahisisha biashara mtandao na kukuza uchumi wa Taifa;

iii) Kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii; Kwa mfano, usajili wa mali, biashara, vizazi na vifo n.k

iv) Kuongeza Usalama wa wananchi kwa kutoa huduma za dharura kwa wakati mfano ajali, moto, ugonjwa na uhalifu;

v) Kuongeza mapato ya Serikali kwa kuwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato zinakuwa na taarifa ya mahali walipa kodi/ wananchi walipo, hivyo kuleta tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;

vi) Kuboresha utendaji wa taasisi mbalimbali kwa mfano, benki kuwa na uhakika wa mahali wanapopatikana wateja wakati wa mikopo n.k

vii) Kurahisisha utambulisho wa watu wanaoishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

viii) Kuwezesha utambuzi wa mwelekeo na eneo ambalo mtu anahitaji kwenda.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio yanayotarajiwa kutokana na kuendelezwa kwa mradi wa anuani za makazi; changamoto mbalimbali zifuatazo zimeendelea kukabili utekelezaji wa mradi huu: -

i) Ufinyu wa Bajeti; hakuna fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na hata kiasi kidogo kinachotengwa hakitolewi chote/ ama kutotolewa kwa wakati; kwa mfano katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kati ya **Shilngi Bilioni 3** zilizoidhinishwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2018 zilitolewa jumla ya **Shilingi 1, 292,279,295.67** tu;

ii) Barabara/ mitaa mingi kutokuwa na majina yaliyorasimishwa;

iii) Uharibifu wa miundombinu ya mfumo uliopo katika miradi;

iv) Kutokuwapo na taarifa za Barabara na Nyumba/ Majengo katika kila Kata na ujenzi holela; na

v) Baadhi ya halmashauri kutokuwa na mpango kazi wa mfumo; na ushirikishaji hafifu wa wadau katika kuchangia gharama za uwekaji wa miundombinu.

x) **Ujenzi wa Mizani Dakawa Morogoro**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa mradi huu ulianza tarehe 25 Oktoba, 2017 na kutarajiwa kumalizika tarehe 24 Oktoba, 2018. Kutokana na changamoto zilizojitokeza, muda wa kukamilika mradi uliongezwa hadi tarehe 24 Machi 2019. Hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2019 kazi ilikuwa imekamilika kwa asilimia 98 ingawa thamani ya kazi iliyoidhinishwa kwa malipo ni asilimia 75. Mradi unagharimu jumla ya **shilingi 14,784,337,526.99** unahusisha ujenzi wa mizani mbili kubwa na za kisasa za kupima uzito wa magari yakiwa katika mwendo; ukiwemo mfumo wa kuchambua magari yaliyozidisha uzito. Mradi huu ni muendelezo wa hatua za kudhibiti na kupunguza uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kuzidisha uzito.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa jumla, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa

miradi hasa ya sekta ya Uchukuzi ni kutopatikana kwa fedha za miradi kwa wakati.

## 2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na: -

a) Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam;
Kamati imejulishwa kuwa hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuondoa vikwazo visivyo vya lazima katika bandari zetu; kama vile kuweka vituo vitatu vya ukaguzi wa maroli kwenye ushoroba wa kati*;* kuiondoa nchi ya DRC Congo kwenye utaratibu wa himaya moja ya forodha, kwa kuwa, nchi hiyo si moja ya mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuanzisha vituo vya pamoja mipakani na kuboresha reli na barabara zilizopo bandarini.

i) Uboreshaji wa gati namba 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magari. Ujenzi wa gati namba 1 umekamilika hapo tarehe 8 Disemba, 2018; ujenzi wa gati la kushushia shehena za magari ambao unahusisha kazi za ujazaji wa kifusi na kuchimba kwa ajili ya kuongeza kina imefikia asilimia 45; Kazi za usanifu wa gati namba 4-7; pamoja na, utengenezaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kujenga na kuimarisha gati namba 2-7 zinaendelea.

ii) Kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli*.* Kazi ya usanifu wa kina ilianza mwezi Disemba 2018 na inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2019. Kazi ya kupanua, kuchimba na kuongeza kina cha lango la kuingilia na kutokea meli zinatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2019.

b) Kampuni ya Huduma za Meli- MSCL, imezingatia ushauri wa kufunga mfumo wa kukata tiketi kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu ulianza rasmi mwezi Januari, 2018 utasaidia kuimarisha njia za ukusanyaji mapato.

c) Ushauri wa kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake yote;

Kamati imefahamishwa kuwa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa ni wa awamu. Awamu ya kwanza utekelezaji wake umefikia asilimia arobaini na na sita (46%) kutoka Dar es Salaam-Morogoro (km 300) na unatarajia kukamilika Novemba, 2019;

Aidha, Awamu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutopora (km 336), Mkataba umesainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na ujenzi wake ulianza 26 February, 2018 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2020. Ujenzi wa reli hii umefikia asilimia saba (7%);

d) Ushauri wa kukarabati na kufufua njia nyingine za reli

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu reli ya Tanga-Arusha- Musoma, ukarabati wa sehemu ya Tanga-Arusha (Km 439), jumla ya Km 253 (Tanga-Mombo-Same), kazi za ukarabati wa njia zmekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa madaraja na makalavati. Aidha, Kuhusu reli ya Mtwara-Mbambabay na Matawi ya Liganga na Mchuchuma, usanifu wa awali wa njia ya reli kwa kiwango cha *standard gauge* umekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukarabati wa baadhi ya maeneo korofi ya reli, madaraja na mabehewa 40 ya mizigo, Shirika la Reli Tanzania limefanikiwa kusafirisha tani 429.994 za mizigo ikilinganishwa na tani 351,758 zilizosafirishwa kwa kipindi cha mwaka 2017 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 22.24**.

e) **Mheshimiwa spika,** Ulipaji wa madeni ya wafanyakazi wa TAZARA; Kamati imejulishwa kuwa kazi ya uhakiki wa madeni ambayo TAZARA inadaiwa ilifanywa na wataalamu kutoka Hazina na kukamilika mwezi February, 2019. Aidha hadi kufikia June 2018 deni la TAZARA lililohakikiwa ni **shilingi biloni**

**433.9**. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kulipa deni linalohusu upande wa Tanzania.

f) **Mheshimiwa Spika,** Kuimarisha usalama wa usafiri wa nchi kavu;

Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kupitia SUMATRA imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali ili kubaini vyanzo vikuu vya ajali za barabarani. Matokeo ya tafiti hizo yanaonesha asilimia 76 ya ajali zinasababishwa na makosa ya kibinadamu, asilimia 16 ubovu wa magari na aslimia 8 ni miundombinu na mazingira. Katika hatua za kutatua changamoto hizo Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kutoa taarifa za mwenendo wa mabasi ya abiria yanayofanya safari za mikoani na kuunganishwa na mfumo unaofuatilia mwenendo wa mabasi (*vehicle tracking system*). Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya mabasi 3083 yalikuwa yamefunga vifaa hivyo. Aidha, Bunge lilitunga Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini, 2018 ambayo imeweka utaratibu wa kusajili wahudumu wote wa vyombo vya usafiri ardhini; kudhibiti taaluma ya udereva na ubora wa vyombo vya usafiri ardhini ambapo ilianza na magari yanayotumika na abiria.

g) **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania;

i. Kuhusu kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Kamati imejulishwa kuwa kazi ya uboreshaji wa kiwanja hiki inaendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la mizigo ambao umekamilika kwa **asilimia 90** na ujenzi wa jengo la kuongozea ndege *(contol tower)* umekamilika kwa **asilimia 90**. Mamlaka inaendelea kufanya marejeo ya usanifu wa ujenzi wa jengo la abiria. Pia Serikali tayari imeanza mazungumzo na Serikali ya Rwanda ili Rwanda Air ianze kusafirisha minofu ya samaki kwenda Ulaya kupitia kiwanja hiki; na

ii. Ulipaji wa fidia ili kumaliza migogoro na wananchi walio kwenye maeneo ya viwanja vya ndege. Kamati ilijulishwa kuwa Serikali imekuwa inalipa fidia kwa wananchi ambao wameathirika kutokana na utwaaji wa ardhi ili kupisha ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini. Serikali imelipa fidia ya **shilingi bilioni 3.4** kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege

Dodoma na **bilioni 4.3** katika viwanja vya ndege vya Sumbawanga na Shinyanga. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS imetayarisha vitabu vya uthamini kwa ajili ya fidia katika viwanja vya ndege vya Songea, Dodoma (awamu ya tatu), Msalato, Simiyu, Lake Manyara, Iringa, Musoma, na Nachingwea. Taratibu za malipo hayo zinaendelea.

h) Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL;
Kampuni imefanikiwa kuingia katika Mfumo wa (*International Air Transport Association-IATA)* na kujiunga na Mfumo wa uuzaji wa tiketi ulimwenguni *(Global Distribution Systema-GDS).* Kwa sasa tiketi za ATCL zinapatikana kwa Wakala wote waliosajiliwa katika Mfumo wa wauzaji wa tiketi duniani.

i) Kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa ambayo bado hayajaunganishwa kwa barabara za lami; barabarara zimeendelea kutengenezwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha, barabara hizo ni barabara ya Kigoma – Kagera, Katavi – Kigoma, Kigoma – Tabora, Katavi – Tabora, Njombe – Mbeya, Arusha – Mara na Shinyanga – Simiyu – Mwanza na Mara.

j) Uharibifu wa barabara kutokana na uzito mkubwa wa mizigo. Kamati imejulishwa kuwa utafiti uliofanywa na chuo kikuu cha Dar Es Salaam kupitia BICO, M/S COWI, CML pamoja na PADECO kupitia JICA ulionesha kwamba matairi ya *super single* yamekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa barabara. Ili kutatua changamoto hii Serikali imeanza kutumia sheria mpya ya udhibiti wa uzito wa mgari ya Afrika Mashariki kuanzia mwezi Machi, 2019 ambapo matairi aina ya *super single* yamepunguziwa uzito wa kubeba mzigo kutoka tani 10 hadi tani 8.5.

Aidha, ujenzi wa mizani bandarini kwa ajili ya kuhakikisha magari yote yaliyozidi uzito hayataruhusiwa kuanza safari kabla ya uzito huo kupunguzwa kwa mujibu wa sheria ya Afrika Mashariki. Kutoa adhabu kali kwa wafanyakazi wa mizani na wasafirishaji wasio waaminifu kwa kuruhusu magari yenye uzito mkubwa kuendelea na safari pale yanapoonekana yamezidisha uzito. Pia ufungaji wa mfumo (*weigh Bridge Management System)* kwa ajili ya kuangalia

utendaji wa mizani zetu kwa uwazi zaidi ili kupunguza rushwa na kuongeza ufanisi.

k) Kupunguza msongamano jijini Dar Es Salaam kwa kujenga barabara za juu hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile Magomeni, Morocco na Mwenge. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa *interchange* kwenye makutano ya Ubungo na ujenzi wa *flyover* mbili katika maeneo ya makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa pamoja na makutano ya barabara ya Kilwa na Nelson Mandela eneo la uhasibu katika mradi wa BRT II ambapo mkataba wa kuanza ujenzi huu umesainiwa.

l) Kuongeza mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo; Kamati imejulishwa Serikali imeendelea na ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa katika mwendo katika maeneo mbalimbali kama vile Dakawa morogoro ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 98, Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe);

m) Serikali kuhakikisha inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (infrastructure sharing) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mrundikano wa minara eneo moja. Kamati imejulishwa kuwa Serikali kupitia mamlaka ya mawasiliano inaendelea kusimamia kuwepo kwa ushirikiano wa miundombinu baina ya watoa huduma na ili kuhakikisha suala hili linatekelezwa ipasavyo serikali ilitunga kanuni za kieletroniki za mawasiliano na Posta (the electronic and postal communications Access, Co-Location and Infrastructure sharing Regulations, 2018). Aidha watoa huduma za mawasiliano wanashirikiana katika matumizi ya pamoja ya minara.

n) Ushauri wa Kamati kuhusu Serikali kufuta deni la **shilingi bilioni 26** ambalo Shirika la Posta linadaiwa na Mamlaka ya mapato Tanzania. Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kupitia Sheria ya Msamaha *(Amnesty)* imekubali kufuta deni la shirika la **shilingi 12,039,071 437** linalotokana na tozo, riba, na adhabu na kubakiwa na deni la msingi la **shilingi 14,840,500,596**. Serikali kupitia wizara ya fedha na mipango inaendelea na taratibu za kuchukua deni hili.

o) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao. Kamati imejulishwa kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai. Kabla ya udhibiti huu Serikali ilikuwa ikipoteza mapato yake kwa asilimia 100. Katika kipindi cha Julai 2018-Februari, 2019 TCRA imefanikiwa kupunguza mawasiliano ya ulaghai kutoka asilimia 15 hadi kufikia chini ya asilimia 5.

## 2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

### 2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan Sekta ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 68,828,000.00** kutoka Idara zenye vyanzo vya mapato kama vile Idara ya Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi. Aidha, Sekta ya Mawasiliano inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 22,517,437,400** katika mwaka wa fedha 2019/2020 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni.

### 2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 4.8 (4,888,087,065,163)**. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa:

**Jedwali Na.2, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida Na Miradi ya Maendeleo Kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

| SEKTA | MATUMIZI YA KAWAIDA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|
| **Ujenzi (Fungu 98)** | 36,142,664,000.00 | 1,204,037,604,268.00 | **1,240,180,268,268** |
| **Uchukuzi (Fungu 62)** | 85,408,131,000 | 3,543,722,242,895 | **3,629,130,373,895** |
| **Mawasiliano (Fungu 68)** | 3,973,197,000 | 15,000,000,000 | **18, 856, 423, 000** |
| **JUMLA KUU** | **125,523,992,000** | **4,762,759,847,163** | **4,888,087,065,163** |

***Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika***,* kwa ujumla Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 kiasi cha **Shilingi Trilioni 4.8** ni ongezeko la **asilimia 14** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha uliopita 2018/2019 ambayo ilikuwa **Shilingi** T**rilioni 4.2.**

### 2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019*/2020*

a) **Sekta ya Uchukuzi**

i. **Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya vipaumbele vikuu kwa upande wa uimarishwaji wa miundombinu ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge).* Katika kufanikisha azma hiyo Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya mradi huu mwaka hadi mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ujenzi wa reli ya kati kutoka **shilingi trilioni 1.5** zilizoidhinishwa 2018/2019 hadi **shilingi trilioni 2.4** zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 60**. Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa kutoka Dar es Salaam- Makutupora – Tabora- Isaka Rusumo.

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hii yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na na usafirishaji wa mali ghafi hatimaye kuchochea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza Pato la Taifa.

Ni matarajio ya Kamati kuwa reli hii itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele kitawekwa katika maeneo ambayo yana mali ghafi nyingi ili kuleta tija.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imejulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Maendeleo ya Reli umetengewa **shilingi bilioni 255.7** (**255,700,000,000)** kwa ajili ya kukarabati reli iliyopo, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya reli za ni Kaliua-Mpanda-Karema, Tabora-Kigoma, Tanga-Arusha-Musoma na Mtwara Mbambabay na matawi ya mchuchuma Liganga.

ii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Majukumu ya Mamlaka hii ni kuendeleza, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji za uendeshaji wa bandari nchini.

Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

Kamati, katika kutekeleza majukumu yake imeelezwa changamoto ambazo zimekuwa zikiikabili Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA kuwa ni: -

a) Uwezo mdogo wa kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga;

b) Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini; na

c) Uchakavu wa Miundombinu ya bandari na reli inayounganisha bandari na maeneo mengine

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa bandari kavu eneo la Ruvu (Vigwaza), katika Vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Machi, 2019, imeelezwa kuwa awamu ya kwanza ya mradi huu imeshakamilika na sasa awamu ya pili imefikia asilimia sabini (70%) na inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019.

Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, katika mwaka wa fedha 2019/2020 imepanga kukamilisha ukarabati na uboreshaji wa magati yaliyoko bandari ya Tanga, ujenzi wa magati katika mwambao wa bahari ya Hindi, kukamilisha ujenzi wa magati katika maziwa makuu, kuendelea na kukamilisha mpango wa utwaaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu katika maeneo ya Katosho, Kibirizi, Chongoleani na Ihumwa Dodoma.
Vilevile, ni muhimu pia kwa bandari zilizo katika kipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani Bagamoyo na Bandari ya Mwambani Tanga kuanza kutekelezwa.

iii. **Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

**Mheshimiwa Spika**, japokuwa Serikali imekuwa na dhamira ya kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu yaani (Victoria, Tanganyika na Nyasa), kwa kununua meli mpya na kukarabati meli zilizopo, bado kumeendelea kuwapo na changamoto mbalimbali ambazo zimesababisha katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, Wakala wa Huduma za Meli kutokufikia malengo iliyojiwekea.
Changamoto kubwa imekuwa kutokutolewa kwa wakati fedha zilizoidhinishwa ambapo katika Mwaka wa fedha 2018/2019 ilitengewa **shilingi bilioni 20**, hadi kufika Machi, 2019 zimetolewa **shilingi bilioni 3** sawa na asilimia 15 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Upungufu huo wa fedha, umesababisha Kampuni ya Huduma ya Meli kufanya kazi chini ya malengo ilichojiwekea Mfano; kusafirisha jumla ya abiria 64,709 ikilinganishwa na lengo la kusafirisha abiria 82,159 ambao ni upungufu kwa abiria 17,450 sawa na asilimia 21.24. Aidha, kwa upande wa mizigo jumla ya tani 15,421 zilisafirishwa katika maziwa yote matatu ikilinganishwa na lengo la kusafirisha tani 68,352 ikiwa ni upungufu wa tani 52,931 sawa na asilimia 77.

iv. **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege kutoka ndege moja iliyokuwepo 2016 hadi kufikia ndege sita. Katika kuendeleza juhudi hizo mwaka wa fedha 2019/2020 zimetengwa **shilingi Bilioni 500 (500,000,000,000)** kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege ya pili aina ya Boing 787 Dreamliner, kukamilisha ndege nyingine aina ya Bombadier Q400 na malipo ya awali ya kununua ndege mbili mpya aina A220-300, ununuzi wa ndege moja Bombadier Q400, ununuzi wa Injini ya akiba kwa ajili ya Bombadier Q400, kuboresha karakana ya KIMAFA na kulipa madeni yaliyohakikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kuongezeka kwa ndege kumeiwezesha Kampuni kuongeza idadi ya miruko ili kukidhi mahitaji ya usafiriwa anga katika baadhi ya vituo kikiwepo kituo cha Dodoma ambapo ndege ilikuwa inafanya safari mara tatu kwa wiki na sasa inafanya safari mara nne kwa wiki. Hadi kufika Desemba, 2018 ATCL imefanikiwa kumiliki soko la usafirii wa anga kwa asilimia 40.8 na kuwa Kampuni inayoongoza kwa soko la ndani.

Aidha, ATCL imeongeza safari za kikanda kuelekea Entebe-Uganda na Bujumbura-Burundi. ATCL imelenga kuongeza safari za Johannesburg, Harare na Lusaka. Vilvile kuanza safari za Kimataifa katika vituo vya Guangzhou, Bangkok na Bombay.

Changamoto zinazoikabili ATCL ni pamoja na uchache wa wataalam hususan marubani, uchache wa nyenzo za kiutendaji hususan magar na madeni ambayo yameendelea kulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

## b) Sekta ya Ujenzi

### i) Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya ujenzi ni sekta muhimu ambayo imekuwa ikitekeleza majukumu mbalimbali ya ujenzi ikiwemo ujenzi ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; Ujenzi ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; Usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; Usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuna upungufu wa **shilingi 772,404,748,873.38** ambazo ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2018/2019 ni upungufu wa **asilimia (39.08)**. Kutokana na upungufu huu wa fedha za miradi ya maendeleo, Kamati inaona hali hii itaathiri ujenzi wa miundombinu hasa

barabara ambazo ndiko kuna watumiaji wengi ukizingatia kwamba barabara ni sekta mtambuka. Vilevile, upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo utaathiri miradi iliyokuwa imeanza na inayoendelea ikiwa ni pamoja na miradi ya kuunganisha baadhi ya Makao Makuu ya Mikoa, ujenzi wa barabara za kiuchumi na barabara za kiusalama.

ii) **Miradi ya ujenzi wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, barabara ni sekta mtambuka kwa kuwa jamii yote hutegemea miundombinu ya barabara ili kufanikisha masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Miundombinu ya barabara inapokuwa mizuri husaidia jamii kwa kurahisisha watu kutoka sehemu moja hadi nyingine, kuokoa muda, gharama na uchovu. Pamoja na umuhimu huo ujenzi wa barabara umekuwa na changamoto kubwa ya kibajeti kwa kutengewa fedha kidogo na kutotolewa fedha kwa wakati. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019, hadi kufikia mwezi Machi, 2019 fedha zilizoidhinishwa kwa baadhi ya miradi ya barabara hazikuwa zimetolewa. Mfano, barabara ya Dar es Salaam-Chalinze–Morogoro express way, Nangurukuru- Mbwemkuru; Dumila- Kilosa-Mikumi; Dumila-Rudewa; Korogwe-Handeni; Singida-Babati-Minjingu; Same- Mkumbara-Korogwe; na Handeni-Kibereshi-Kibaya-Singida.

Aidha, baadhi ya barabara fedha zilitolewa kidogo ukilinganisha na kiasi kilichoidhinishwa na muda uliobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2018/2019. Barabara hizo ni Wazo Hill -Bagamoyo- Msata; Usagara-Geita-Buzirayombo- Kyamyorwa; Dodoma -Manyoni;

Sumbawanga -Mpanda-Nyakanazi; Ipole-Rungwa; na Magole-Mziha-Handeni.

**Mheshimiwa Spika**, lengo mojawapo la Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha Miji yote Mikuu na Mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami. Hata hivyo, bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya –Makete- Njombe, Lindi- Morogoro, Lindi-Ruvuma n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

iii) **Malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wakandarasi na Wahandisi Washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2019 deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **shilingi bilioni 711.13**. Madeni yaliyolipwa ni yale yaliyohakikiwa hadi mwezi Juni, 2016 ambapo kiasi cha **shilingi trilioni 1.6** zimeshalipwa. Aidha, kazi ya kuhakiki madeni ya hadi mwezi Juni, 2017 imekamilika na fedha zinaendelea kutolewa kwa ajili ya malipo ya madai ya miradi ya barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wakandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 442,005.782** za Mfuko wa Barabara zimetumika kulipa Makandarasi wa ndani. Hata hivyo, changamoto kubwa imeendelea kuwa uwezo mdogo wa mtaji walionao Makandarasi wa ndani hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi, mitaji ya kuwezesha kufanya kazi kutoka mabenki kuwa ngumu na kutozingatia mahitaji halisi ya shughuli za kuhandisi. Hali hii ya kukosa mitaji kunawafanya

Makandarasi kushindwa kukua na kupata fursa ambazo zitawezesha kuwakwamua kutokana na uwezo mdogo.

iv) **Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Machanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pikipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye weledi unaoenda sambabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa vinavyoweza kuendana na magari ya kisasa na mitambo ya kisasa ambayo inahitaji kutumia mashine ili kugungua tatizo wakati wa ukarabati. Kutokana na changamoto hizo, magari ya Serikali yanakwenda kutengenezwa kwa waagizaji wakubwa *(dealer)* ambao gharama zao zinatozwa kulingana na muda ambao umetumika kutengeneza gari husika na hivyo kusababisha gharama kuwa kubwa.

v) **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, miradi mbalimbamli ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika Mikoa mbalimbali kama vile Kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe. Kazi kubwa zinazofanyika katika miradi hiyo zinajumuisha ujenzi barabara za ndege, upanuzi wa barabara za ndege, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa vituo vya uangalizi wa hali ya hewa, ujenzi wa barabara za kuingilia viwanja vya ndege, uboreshaji wa viwanja hivyo pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria na mizigo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2019, mradi wa kiwanja cha ndege cha Julius nyerere ulikuwa umekamilika kwa asilimia tisini na tano (95%) na viwanja vingine vya ndege miradi bado inaendelea. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Arusha na Kilimanjaro vinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti hali inayosababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hii.

**Mheshimiwa Spika**, kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

vi) **Sekta ya Mawasiliano**

**a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeweka Mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu *(Tele-Traffic Management System-TTMS)*, ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano. Mkataba ulikuwa wa miaka mitano ambao uliingiwa kwa njia ya Kujenga, Kuendesha na Kuhamisha Umiliki *(Build, Operate and Transfer).* Mkataba ulianza 1 Oktoba 2013 na umemaliza muda wake tarehe 30 Septemba, 2018. Toka mfumo huu ulipoanza kufanya kazi mpaka Septemba 2018, Serikali imeweza kupata chanzo kipya cha mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za Kimataifa zinazoingia nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 93,665,645,344.55** ziliwasilishwa Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasilinao duniani.

**b) Mradi wa Postikodi na Misimbo za Posta**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni muhimu sana kutokana na faida zake kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa mradi huu, bado kumeendelea kuwapo changamoto ya kutokutolewa fedha za maendeleo kwa wakati hivyo kusababisha mradi kutekelezwa ipasavyo. Kwa miaka mitatu mfululizo mwenendo wa utoaji fedha katika mradi huu sio wa kuridhisha. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95** tu; katika mwaka wa fedha wa 2017/18 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi bilioni 4** lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichopokelewa na kutumika ni **shilingi milioni 796** tu.

c) **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(Universal Communication Service Access Fund- UCSA*F) ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2006 ukiwa na lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya simu kama vile TIGO, VODACOM, HALOTEL.

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo mwezi Julai, 2018, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua minara ya mawasiliano ya simu iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote- UCSAF na kwa ushirikiano na Makampuni binafsi. Lengo la ziara hii lilikuwai kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa mawasiliano hasa katika maeneo ya pembezoni ambayo Serikali imetoa fedha zake (ruzuku). Ziara hii ilijumuisha Mikoa kumi na mbili (12) ya Tanzania Bara ambayo ni Morogoro, Tanga,

Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Simiyu, Shinyanga, Iringa, Njombe, Ruvuma na Lindi.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo, yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ziara hiyo: -

i) Ushiriki wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano; Pamoja na Serikali kutoa ruzuku za ujenzi wa minara ili kuhakikisha mawasiliano yanawafikia watu wote, hakuna alama yoyote iliyowekwa katika minara kutambulisha wananchi na jamii mchango wa Serikali. Hili linafanya mchango wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano kutojulikana kabisa na badala yake Makampuni husika ndio yanayoonekana na kufahamika kutoa huduma hiyo muhimu.

ii) Umiliki wa Maeneo yaliyojengwa Minara; Taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa minara kutokuwa wazi jambo linalosababisha Serikali za Vijiji husika kutokunufaika kwa namna yoyote na malipo ya pango la eneo lililojengwa mnara. Kamati imebaini kuwa watu binafsi ambao si wakazi wa vijiji husika ndio walionunua maeneo hayo na kupangisha Makampuni ya simu.

iii) Ushiriki katika Kazi za Maendeleo; Makampuni ya Simu hayashiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo *(Corporate Social Responsibility)* katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibiashara mathalani maeneo ambayo wamejenga minara.

iv) Kutokuwepo Mawasiliano wakati Wote; Kamati imebaini pamoja na kuwepo kwa minara, upatikanaji wa huduma ya simu kwa wananchi wa baadhi ya vijiji vilivyotembelewa imekuwa si wakati wote kama ambavyo Serikali imekusudia. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; minara kuwepo mbali na watoa huduma, minara kujengwa katika vilima ambapo hakuna miundombinu ya barabara za magari kufikisha huduma jambo linalosababisha ucheleweshwaji wa

huduma ya matengenezo au mafuta ya *generator* na kusababisha kukosa mawasiliano na uelekeo wa mnara na uwepo wa milima inayozuia za mawasiliano kufika katika vijiji vilivyokusudiwa.

v) Utunzaji wa Mazingira; Kamati imebaini kuwa maeneo yaliyojengwa minara inayomilikiwa na Kampuni ya Tigo (MIC), Vodacom na Halotel hakuna huduma za msingi kama vile chumba cha kulala na choo cha mlinzi. Jambo hili si sahihi na huchangia uchafuzi wa mazingira kwani walinzi hujisaidia vichakani na ikiwa mnara upo jirani na makazi ya watu, hulazimika kuomba huduma katika makazi ya wananchi.

Aidha, kutokuwepo kwa nyumba ya mlinzi kumekuwa ni changamoto kubwa kwani maeneo mengine yapo katika hifadhi au mbuga za wanyama na hivyo kuhatarisha maisha ya walinzi wa minara.

vi) Ujenzi wa Minara katika eneo moja; Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wanahitaji huduma za mawasiliano toka kwa watoa huduma mbalimbali kulingana na uchaguzi wa huduma bora. Hata hivyo, kwa matumizi bora ya ardhi, Kamati inaona si sahihi kwa kila Kampuni kujenga mnara wake kwani baada ya muda nchi yetu itakuwa imetapakaa minara ukiachilia mbali miundombinu mingine muhimu.

vii) Uhitaji wa Huduma za ‘‘*Internet”;* Katika maeneo yote ya minara ambayo Kamati imetembelea, kumebainika uhitaji mkubwa wa huduma ya *internet.* Hii ni kutokana na minara mingi iliyojengwa kupitia mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuwa ya kiwango cha 2G ambayo hutoa huduma ya sauti na ujumbe pekee.

viii) Minara Maeneo ya Mipakani; Kumekuwapo na changamoto ya wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kukosa huduma ya mawasiliano au wakati mwingine kupata huduma ya

mawasiliano toka nchi jirani jambo ambalo si sawa na ni hatari kwa usalama wa nchi.

ix) Rasilimali watu katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote**;** Kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali wa kujenga minara, imebainika kuwepo kwa wafanyakazi wachache katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kumekuwa na changamoto hasa katika kufuatilia miradi hiyo wakati wa ujenzi na hata kufuatilia ufanisi wake.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa kusambaza mawasiliano unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha za kutosha kupeleka mawasiliano katika maeneo yenye uhitaji wa huduma hiyo kwa wakati. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja ya Mfuko wa Mawasiliano kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.

**d) Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Shirika la Mawasiliano Tanzania-TTCL, Kamati imejulishwa kuwa Serikali iliruhusu TTCL kukopa **Shilingi Bilioni 96** kwa kutumia dhamana ya rasilimali za Shirika ambapo hadi mwezi Machi 2019, shirika limeshakopa **Shilingi Bilioni 66** na limewasilisha maombi ya kukamilisha mkopo wa kiasi kilichobaki. Fedha hizo zimeiwezesha kampuni kutekeleza majukumu yake kama vile kuendesha huduma ya T-Pesa ambapo hadi mwezi February, 2019 Shirika lilikuwa na wateja 351,000 na jumla ya mawakala 10,000; kuongeza idadi ya wateja hai kutoka wateja 488,537 mwaka 2017/2018 hadi wateja 1,074,642 mwezi February, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali bado Shirika la Mawasiliano Tanzania limeendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ya zamani ambapo hadi kufikia June, 2018, jumla ya **Shilingi Bilioni 28** zilikuwa zinadaiwa kutoka kwa Serikali na Taasisi zake.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Bajeti ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutoka **Shilingi trilioni 4.2** kwa mwaka 2018/2019 hadi **Shilingi trilioni 4.8** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ongezeko la Fedha la takribani **asilimia 14,** fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuna upungufu wa **shilingi 772,404,748,873.38** ambayo ni sawa na **asilimia (39.08)** ya Fedha za miradi ya Maendeleo za Sekta ya Ujenzi zilizokuwa zimeidhinishwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati inashauri Serikali kutafuta fedha hizo zilizopungua takribani **shilingi bilioni 772.4.** Fedha hizi zitasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini ambayo bado imekuwa na changamoto ya kutokupitika wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta ya Mawasiliano, hakuna fedha yoyote iliyotengwa. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zitatolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu fedha hizo zitolewe ili kuendeleza miradi muhimu iliyokuwa inaendelea, kama vile, mradi wa Anuani za Makazi na misimbo ya posta, mkongo wa taifa wa mawasiliano, na ujenzi wa kituo cha kutengeneza Vifaa vya TEHAMA.

3.2 **Sekta ya Uchukuzi**

1. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inashauri yafuatayo;

a) Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika kwa muda mfupi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – kigoma -Uvinza-Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema; na Tabora- Mwanza;

b) Ujenzi wa reli ya Kati uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze;

c) Mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni; pamoja na, uratibu wa matumizi ya reli mpya yatolewe ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia mradi huu;

d) Serikali ihakikishe mradi wa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro unakamilika kwa wakati mwezi Novemba, 2019 kama Mkataba na Mkandarasi unavyoonesha ili kuepuka gharama;

e) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;

f) Shirika la reli lianze kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;

g) Kwa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni wa gharama kubwa, na kwa kuwa; pamoja na ujenzi wa reli ya kati unaoendelea sasa, pia tunatarajia kuanza kujenga reli nyingine za Tanga –Arusha –Musoma (1108 km), Mtwara- Mbambabay na Mchuchuma-Liganga (1092 km) na Isaka – Rusumo (371). Kamati inashauri Serikali kujenga reli hizi kwa awamu kwa kufuata kipaumbele; na

h) Serikali iangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu ili kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

2. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo;

a) Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake;

b) Pamoja na kuwa shughuli za upanuzi na ukarabati wa bandari ya Dara es Salaam unaendelea, Kamati inasisitiza, ili kuongeza ufanisi na mapato katika bandari ya Dar es Salaam, ni vema juhudi za makusudi zifanyike ili kuweza kuhamisha gati la mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga gati namba 13 na 14;

c) Wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia Mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-TBS, Wizara ya Nishati na Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;

d) Serikali iharakishe ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda mrefu sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Fela-

Mwanza, Katosho-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala-Mbeya;

e) Serikali iharakishe kutafuta mwekezaji ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwa kuwa bandari hii ni muhimu na itatoa fursa za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;

f) Serikali iharakishe mchakato wa kupata *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam kwani kutokuwepo na mtambo wa kupima kiasi cha mafuta (*flow meter)* kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam; na

g) Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni. Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA ishirikiane kwa karibu na Shirika la Reli Tanzania- TRC kuona namna ya kuimarisha mtandao wa reli, kwa kuwa bandari hii ikiunganishwa na reli itazalisha mapato makubwa kwa nchi;

3. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL kufunga teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (*Flow Scanner)* na kuweka mfumo wa kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (*trucking system)*. Kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni;

b) Serikali ijipange kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara na hata kuweza kulipa madeni yote inayodaiwa;

c) Kutokana uwekezaji unaofanyika sasa wa kukarabati na ujenzi wa meli mpya katika Maziwa Makuu, ni vema Serikali iendelee kulipa mishahara ya

kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kujiendesha; na

d) Serikali iharakishe kukamilisha zoezi la kurasimisha bandari bubu zilizopo katika mwambao wa bahari ya Hindi na katika maziwa makuu ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya TAZARA kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Nchi Serikali kwa kushirikiana na nchi wabia wa TAZARA ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka china kwa ajili ya kusaidia kuiboresha TAZARA.
b) Seikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza pato la TAZARA.
c) Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa TAZARA ili kupata wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

d) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za ujenzi wa kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kutoka Chikola kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha; na

e) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kulipa deni lote la TAZARA ambalo uhakiki wake umekamilika na kuendelea kutafuta fedha ili kulipa deni hasa linalohusu upande wa Tanzania.

5. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania- TAA: -

a) Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- (TAA) iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati; pamoja na, uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Mamlaka izitumie vizuri fedha za mapato ya ndani zinazotokana na utuaji wa ndege, uegeshaji wa ndege na magari katika maegesho ya viwanja ili ziweze kutumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege;

b) Serikali ihakikishe Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki; Aidha, kuhakikisha Viwanja vya Ndege vyote vinawekewa uzio kwa ajili ya kuepusha hatari zinazotokana na wanyama au binadamu wanaokatiza katika maeneo ya viwanja vya ndege pamoja na; kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaoishi pembezoni mwa viwanja hivyo;

c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na wadau wengine wa viwanja vya ndege kama Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), wafanye vikao vya pamoja na kuangalia namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika sekta ya usafirishaji wa anga;

6. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL,

a) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga.

## 3.3 Sekta ya Ujenzi

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara- TANROADS, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami kama vile, Lindi –Morogoro, Morogoro-Mlimba-Madeke Njombe, Lindi –Songea, Kigoma –Katavi-Tabora-Kagera, Mbeya-Makete-Njombe, Arusha–Mara. Aidha, miradi ya barabara inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu. Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo: -

i. Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;
ii. Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora;
iii. Barabara za Kiuchumi, kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi; ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; na barabara ya Singida – Chemba – Handeni – Tanga ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda. Aidha, umuhimu wa makubaliano ya nchi ya Rwanda kutaka kutumia bandari ya Tanga; na
iv. Barabara zilizohaidiwa za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani.

b) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuchukulia hatua kali kwa wakandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango;

c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa wahandisi washauri na wakandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha wakandarasi wazalendo kujiunga

na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kati;

d) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

e) Serikali iharakishe kuleta Sheria ya Vyuma Chakavu bungeni ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma vya alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vilevile, kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vya alama barabarani;

f) Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

g) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

h) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo, kwani, maeneo mengi ambayo mifugo inatumia kuvuka kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara;

i) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa wakandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira); pamoja na, ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji; gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara, hivyo, Kamati inaishauri Serikali isamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi;

j) Serikali iendelee kutoa kazi za ujenzi wa barabara kwa wakandarasi wazawa ili kuweza kuongeza ujuzi na uzoefu katika shughuli za ujenzi; na

k) Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi, kama vile, Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria. Aidha, ikamilishe ujenzi wa jengo la mizigo; pamoja na, jengo la kuongozea ndege ambayo yote yamefikia asilimia 90. Kamati inasisitiza ushauri huu kutokana na umuhimu wa kiwanja hiki ambapo yapo mashirika mengi ya ndege kama Ethad, Fly Dubai, Rwanda Air, Jambo Jet ya Kenya yameonyesha nia ya kufanya safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na hivyo kukifanya kiwanja hiki kuwa cha kimataifa;

b) Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

c) Serikali iwekeze kwa wataalam wa ndani, hasa, katika kazi za ujenzi; kama vile, shughuli za usanifu wa miradi mbalimbali. Hii itapunguza gharama kubwa ya kuajiri wataalam hao kutoka nje. Vilevile, itasaidia kuimarisha wataalam wetu wa ndani ya nchi. Ni vema wataalam wa ndani, mathalani, wahandisi wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika nchi nyingine duniani ili kuweza kujenga miundombinu ya kisasa kulingana na dunia inavyokwenda;

d) Ni muhimu Serikali ijenge na kuimarisha Viwanja vya Ndege vitakavyozalisha mapato na kujiendesha; kama vile, Kiwanja cha Ndege cha Moshi (kwa ajili ya utalii), Kiwanja cha Ndege cha Iringa (kwa ajili ya Utalii) na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara (kwa ajili ya uwekezaji);

e) Serikali ilipe fidia mapema na kwa wakati kwa wananchi wanaopisha ujenzi mathalani kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Songea, Lake Manyara, Simiyu na Msalato;

f) Serikali iweke taa haraka za kuongozea ndege hususan katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe-Mbeya ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote;

3) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme- TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Wakala uharakishe mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makuu ya Mkoa;

b) Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo, kwa kiasi kikubwa, inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

c) Serikali iajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa

teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

4) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu changamoto ya wakandarasi wa ndani kuwa na mtaji mdogo wa kuwawezesha kufanya kazi, Kamati inasisitiza Wizara; pamoja na, Bodi ya usajili wa wakandarasi kuhamasisha wakandarasi wa ndani kujiunga katika Mfuko Maalum wa Kutoa dhamana ya kusaidia wakandarasi wadogo na wa kati.

### 3.4 Sekta ya Mawasiliano

1) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu mradi wa Anuani Makazi na Misimbo ya Posta, Kamati inashauri yafuatayo; -

   a) Serikali itoe kipaumbele kwa mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

   b) Ili mradi huu uwe wa kisasa na kuendana na wakati, ni vema wataalam wakajifunze nchi zingine na kuona namna nchi nyingine zilivyofanya na kuweka mfumo huu;

   c) Vibao vinavyoonesha majina ya mitaa viandikwe kwa lugha ya Kiswahili; na

   d) Wakati zoezi la kuweka majina ya mitaa linaendelea, ni muhimu Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka ulinzi wa nguzo dhidi ya wahalifu wanaochukua vyuma chavu.

2) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Kamati inashauri; -

a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya uhalifu wa kimtandao na kuwabana wahalifu;

b) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao; na

c) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kamati inashauri

a) Serikali ipitie na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo ya ardhi yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia kwani fedha zitakazopatikana kutokana na malipo kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;

b) Serikali ihakikishe inaweka mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Serikali za Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya chini pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote UCSAF; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa

minara inajengwa na Makampuni ya ya simu yenyewe; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa;

Aidha, wakati wa uzinduzi wa kuwasha minara iliyojengwa kwa ruzuku za Serikali, licha ya kuweka bango la kuonesha mchango wa Serikali; ni muhimu pia kufanya uzinduzi kwa kualika vyombo mbalimbali vya habari ili kujulisha wananchi kazi na maendeleo ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF;

c) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-(TCRA) iwekea masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (Corporate Social Responsibility);

d) Serikali iweke mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kukosa taarifa za nchi yao;

e) Serikali ihakikishe inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (*Infrastructure Sharing)* na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;

f) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka;

g) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara view salama; na

h) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo

Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa;

i) Serikali ijenge miundombinu ya barabara katika maeneo yaliyojengwa minara ili kurahisisha utoaji wa huduma za minara na wananchi kwa ujumla. Vilevile kurahisisha shughuli zingine za maendeleo kama vile utalii, kilimo na hata uwekezaji; na

j) Kwa kuwa teknolojia imeendelea na wananchi wengi wamekuwa na mwamko katika huduma za TEHAMA; na hivyo, kuhitaji huduma ya *data (mtandao)*. Ni muhimu sana, minara yote iliyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe na uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya (afya mtandao), elimu mtandao n.k

k) Serikali ifanye jitihada za kuweka na kusambaza mawasiliano nchini katika maeneo mengi zaidi hasa mipakani kwani mawasiliano ni maendeleo na hasa sasa ambako nchi yetu inawekeza katika viwanda. Kuwepo kwa mawasiliano kutarahisisha usafiri na uuzwaji wa malighafi na mazao hata kuinua kipato cha Mwananchi mmoja mmoja na hata Tiafa kwa ujumla

4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Kamati inashauri yafuatayo: -
   a) Serikali iharakishe kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa deni hilo kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika; na

   b) Serikali iliondoe Shirika la Posta katika orodha ya mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kujiendesha kwa tija;

5) **Shirika la Simu Tanzania- (TTCL Corporation)**
   a) Shirika la Mawasiliano Tanzania- TTC liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kwa Wizara/Taasisi na Mashirika ya Serikali ambayo

madeni hayo yameripotiwa hadi Juni 2018 kufika Jumla ya **Shilingi Bilioni 28**; na

b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa. Hili lifanyike kwa kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu Makampuni ya Simu mengine kumiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Serikali kwani Mikongo hii binafsi itafifisha maendeleo ya Mkongo wa Serikali na hata kuhatarisha usalama wana nchi pamoja na kuikosesha Serikali Mapato;

## 4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, sekta hii ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

### 4.1 **Shukrani**

**Mheshimiwa spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb- M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb

10. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili, Mb
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb
13. Mhe. Ahmed Makbhuty Shabiby, Mb
14. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb
15. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb
16. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb
17. Mhe. Dua William Nkurua, Mb
18. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb
19. Mhe. Agness Mathew Michael, Mb
20. Mhe. Charles Kitwanga, Mb
21. Mhe. Rukia Kassim, Mb
22. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
23. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb
24. Mhe. Munde Abdalah Tambwe, Mb
25. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe, (Mb) akisaidiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Justus Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch.Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonaz. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Vilevile, shukrani ziende kwa Katibu Mkuu Dkt. Leonard M. Chamuriho akisaidiana na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile nachukuwa fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA MIUNDOMBINU**

9 Mei, 2019